

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**  
**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE 2020**

**01 MANENO YA IMLA**

**Maelekezo kwa Msimamizi**

1. Tumia **dakika (15) kumi na tano** kusoma imla kwa wanafunzi katika swali la **1**.
2. Soma maneno ya Imla kwa **sauti** na kwa **umakini**.
3. Waelekeze wanafunzi kuwa utasoma kila sentensi **mara tatu** hivyo wasikilize kwa makini.
4. Soma taratibu sentensi moja **mara tatu** na kuweka **pumziko** la **sekunde 20** ili wanafunzi waweze kuandika maneno uliyosoma.
5. Soma tena maneno **yote** kwa **mara ya mwisho** ili wanafunzi wafanye marekebisho ya maneno waliyokosea kuandika.

## **IMLA**

- i) Fikiri ni mpwa wangu.
- ii) Asante sana mwalimu wetu.
- iii) Baba anakunywa maji mengi.
- iv) Daktari alitushauri tutunze masikio.
- v) Thamani ya elimu imedhihirika.